## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM

Simu Na. +255 (026) 2963341/2963346
Nukushi: +255 (026) 2963348
Barua Pepe: ps@jamii.go.tz
Tovuti: www.jamii.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba
Barabara ya Afya
S.L.P 573,
40478 DODOMA.

## TAARIFA KWA UMMA

### KULAANI VITENDO VYA UNYANYASAJI WA WASAIDIZI WA KAZI ZA NDANI

08 Agosti, 2024

Hivi karibuni kuna video imesambaa kwenye mitandao ya kijamii ikimuonesha binti ambaye ni msaidizi wa kazi za ndani akihojiwa na waajiri wake juu ya tuhuma zinazohusu kuwalisha chakula kichafu na kuchafua nguo za watoto anaowalea katika familia hiyo.

Wizara inakemea na kulaani kitendo cha kumuhoji, kupiga picha na kusambaza kwenye mitandao ya kijamii kwani ni kinyume na Sheria ya Mtoto Sura ya 13 Sehemu ya 33(1).

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 12 cha Sheria ya Mtoto Sura ya 13 ya Sheria za Tanzania, ni kosa la jinai kumwajiri mtoto kwa shughuli yoyote inayoweza kuwa na madhara kwa afya yake, elimu yake, afya yake ya akili au makuzi yake ya kimaadili. Adhabu ya kosa chini ya Kifungu cha 14 cha Sheria hiyo kwa kosa hili ni kifungo hadi miezi sita na faini hadi milioni tano au kifungo na faini kwa pamoja.

Nitumie fursa hii kuwaasa wananchi wote kutofumbia macho vitendo hivi na kutoa taarifa ya matukio kama haya kwenye Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Mtoto zilizopo katika kila Mtaa, Kijiji, Kata na Ofisi za Ustawi wa Jamii kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Dawati la Jinsia na Watoto kwenye vituo vya Jeshi la Polisi Tanzania.

Hatua hizi zitapelekea hatua za kisheria zichukuliwe haraka. Wizara inaomba raia wema wenye taarifa sahihi za Mkoa, Wilaya, Mtaa na Makazi ambapo tukio hili limetokea kutoa taarifa kwa utaratibu huo ulioelezwa hapo juu.

Vilevile, Wizara inasisitiza wananchi kuzingatia sheria na maadili katika kushughulikia suala lolote lile linalohusu watoto.

**Tanzania bila ukatili wa kijinsia, inawezekana!**

Gwajima

Dkt. Dorothy Gwajima
**Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.**